# Tani 3,874,055 za sulphur zimeingia nchini kwa miaka mitano

Na Mwandishi Wetu,
*DAR ES SALAAM*

MAMLAKA ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) imesema jumla ya meli 112 zenye tani 3,874,055 za sulphur zimeingia nchini tangu mwaka 2021 ambapo sheria ya kuingiza kemikali hiyo ilipoanza kufanya kazi.

Akizungumza jana wakati wakufungua kikao cha waingizaji,wahifadhi na wasafirishaji wa kemikali aina sulphur kwa niaba ya Mkemia Mkuu wa Serikali Dk.Fidelice Mafumiko,Mkurugenzi wa Huduma ya Udhibiti Daniel Ndiyo alisema kemikali hiyo inaingizwa nchini na kusafirishwa kwenda nchi za Jamhuri ya Demokrasi ya Congo na Zambia.

Alisema kemikali aina sulphur inatumika katika nchi hizo kwa ajilinya utengenezaji wa Copper hali hiyo imesababisha Tanzania kupitisha mzigo mkubwa wa sulphur.

"Miaka ya nyuma mzigo wa namna hii ulikuwa hauruhusiwi kuingia nchini lakini mwaka 2019 Bunge ilibadilisha sheria ikaruhusu,2020 zikatungwa kanuni kuanzia Julai 2021 tukaanza kuingiza sulphur.

"Tangu kipindi hicho jumla ya meli 112 zimeingizwa tani 3874,055 kwa wastani meli moja inaweza kuingiza mpaka Sh Bilioni moja,biashara hii kwa sasa inatuingiza fedha pamoja na kwamba ilikuwa hairuhusiwi,ukipiga mahesabu ya tani ya sulphur moja inabeba malori 100 ambayo wananchi wanapata ajira,"alisema Ndiyo.

Alisema mpaka sasa kuna wasafirishaji wa sulphur 212 wanaotambulika na kwamba kwa muda wa miaka miwili jumla ya ajali 62 zilitokana na sulphur zimerekodiwa katika malori zaidi ya 100

Alisema hivyo kutokana na ukubwa wa biashara hiyo GCLA kwakushirikiana wasafirishaji wanaangalia namna ya kuweka njia bora za usafirishaji kwa utaratibu mzuri na usalama.

"Tunataka kuangalia namna tunaweza kuboresha usafirishaji wa sulphur inaingia nchini si kwa matumizi ya nchini ni ya DR

Ni mzigo ambao unachangia kuingiza kipato kwa bandari ya Dar es Salaam na Tanga,GCLA tuliweka taratibu za upakuaji na tahadhali ili isije kuwaka moto kwakuwa sifa ya sulphur ni kuwaka moto lakini sasa tunataka kuona njia bora zaidi za usafirishaji,"alisema Ndiyo.

Alisema kikao hicho kitajadili matakwa ya sheria na kanuni pamoja na kuziboresha na kuhakikisha wanatimiza matakwa ya kanuni kwakuwa biashara hiyo ina faida kubwa .

"Wakienda na sulphur wanarudi na copper kwa hiyo bandari yetu inatoa mzigo,tunataka kujadili changamoto pamoja na kuboresha na kuendeleza biashara hiyo,hakuna kitu ambacho kimenyooka lazima kiwekwe sawa,"alisema.

Naye mwakilishi wa kampuni ya DSM Corridor Group Limited Mhandisi George Alando alisema kama kampuni wamekuwa wakufanya mafunzo mbalimbali kwa madereva yakuhifadhi sulphur.

"Unahifadhi sulphur na kuifanyia packaging baada ya hapo zinasafirsihwa kwemda Zambia na DRC,tunafuata muongozo uliotolewa na ofisi ya mkemia na tunaandaa tararibu zetu kama ofisi," alisema.

# DCEA:Wakulima wamepunguza kulima bangi Mara

Na Mwandishi Wetu,
*RORYA*

KAMISHNA Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Aretas Lyimo, amesema kilimo cha bangi katika Mkoa wa Mara kimepungua kwa takribani asilimia 80 kutokana na operesheni endelevu zinazotekelezwa na Serikali katika kukabiliana na uzalishaji wa dawa za kulevya.

Akizungumza jana, baada ya kuhitimisha operesheni maalumu zilizofanyika katika Wilaya za Tarime na Rorya, Lyimo alisema operesheni hizo zimefanikisha kuteketezwa kwa mashamba ya bangi yenye ukubwa wa ekari 291.2, kukamatwa kwa magunia 15 ya bangi kavu pamoja na pikipiki nne zilizokuwa zikitumika katika shughuli hizo haramu. Aidha, watu wawili wamekamatwa huku uchunguzi ukiendelea kuwabaini na kuwakamata washirika wengine waliohusika katika mtandao huo.

Alisema mafanikio hayo yanathibitisha ufanisi wa operesheni za Serikali, akibainisha kuwa mwaka 2024 zaidi ya ekari 3,500 za mashamba ya bangi ziliteketezwa katika Mkoa wa Mara. Hatua hiyo, alisema, imechangia kwa kiwango kikubwa kupunguza uzalishaji wa bangi na kudhoofisha mtandao wa kilimo hicho katika maeneo yaliyokuwa yakiathirika zaidi.

"Matokeo haya yanaonesha kuwa juhudi za Serikali zinaendelea kuzaa matunda. Wananchi wengi wameanza kuachana na kilimo cha bangi na kuelekeza nguvu zao katika shughuli halali za uzalishaji zinazowanufaisha wao, familia zao na Taifa kwa ujumla," alisema Lyimo.

Kamishna Jenerali amewataka wananchi ambao bado wanajihusisha na kilimo cha bangi kuachana na shughuli hiyo mara moja na kuwekeza katika kilimo halali cha mazao ya chakula na biashara. Aidha, aliwahimiza kuendelea kushirikiana na DCEA na vyombo vingine vya dola kwa kutoa taarifa za siri kuhusu watu wanaojihusisha na uzalishaji, usafirishaji na biashara ya dawa za kulevya.

Alisisitiza kuwa DCEA itaendelea kuimarisha operesheni, doria na uchunguzi wa kina katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya wote watakaobainika kujihusisha na makosa ya dawa za kulevya.

Kwa upande wake, Afisa Tarafa wa Nchaje, Stephano Peter Kiabaroti, alisema uwekezaji unaoendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan umeongeza uwezo wa DCEA kutekeleza operesheni zenye matokeo makubwa katika kudhibiti na kutokomeza kilimo cha bangi.

Alisema wananchi wengi waliokuwa wakitegemea kilimo hicho sasa wamehamia katika uzalishaji halali wa mazao ya chakula na biashara pamoja na shughuli za ufugaji, hatua ambayo imeanza kuleta manufaa ya kiuchumi kwa familia na jamii kwa ujumla.

Naye Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Rozana, Bi. Kurwa Robert, alisema kabla ya operesheni hizo matumizi na biashara ya bangi vilichochea ongezeko la vitendo vya uhalifu, huku baadhi ya vijana wakijihusisha na makundi ya uhalifu na kujichukulia sheria mkononi.

Alisema baada ya DCEA kuimarisha operesheni za kuteketeza mashamba ya bangi, hali ya usalama imeimarika kwa kiasi kikubwa na wananchi wameanza kurejea katika shughuli zao za kila siku kwa utulivu.

Kwa upande wake, Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Nkerege, Joseph Mwita Ryoba, alisema kijiji hicho kilikuwa miongoni mwa maeneo yaliyoathirika zaidi na kilimo cha bangi, ambapo mwaka 2024 zaidi ya ekari 3,000 ziliteketezwa katika operesheni za Serikali.




*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Mahusiano Mhe. Deus Sangu, akihutubia waumini na wageni mbalimbali wakati wa Maadhimisho ya Kumbukizi ya Damu ya Yesu (C.PP.S) ya Provinsi ya Tanzania yaliyofanyika katika Viwanja vya Parokia ya Kupaa Bwana Wilaya ya Manyoni, mkoani Singida.*

# SERIKALI YAZINDUA MRADI WA MIKOPO NAFUU UJENZI WA VITUO VIDOGO VYA MAFUTA VIJIJINI

Na Mwandishi Wetu,
*DAR ES SALAAM*

SERIKALI kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kwa ushirikiano na Benki ya Azania imezindua rasmi mradi mkubwa wa utoaji wa mikopo nafuu kwa wajasiriamali wadogo, utakaofanikisha ujenzi na uendeshaji wa vituo vidogo vya kuuza mafuta ya petroli na dizeli maeneo ya vijijini.

Hatua hiyo inalenga kuongeza upatikanaji wa nishati ya mafuta, kupunguza gharama zisizo za lazima kwa wananchi na kuchochea ukuaji wa uchumi katika maeneo hayo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya utiaji saini wa mikataba kwa wanufaika nane wa kwanza, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati (Mafuta na Gesi), Dkt. James Mataragio, alisema serikali imeamua kusogeza huduma hiyo karibu na wananchi ili kumaliza changamoto ya kutembea umbali mrefu kufuata nishati hiyo.

"Mafuta ni nguzo muhimu ya maendeleo ya uchumi na ustawi wa jamii. Mpango huu utasaidia kupunguza tofauti kubwa ya bei kati ya mijini na vijijini, ambapo awali maeneo mengine wananchi walilazimika kununua mafuta kwa bei inayozidi mara mbili ya ile ya mijini," alisema Dkt. Mataragio.

Dkt. Mataragio aliongeza kuwa ujenzi wa vituo rasmi utaondoa hatari za moto na ajali zinazotokana na uuzaji au uhifadhi wa mafuta kwenye chupa za plastiki na magaloni yasiyokidhi viwango vya usalama.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi, Hassan Saidy amesema baada ya mafanikio makubwa ya kupeleka umeme vijijini, sasa Wakala umefungua ukurasa mpya wa kusambaza huduma za mafuta katika maeneo ambayo kwa muda mrefu hayajapata uwekezaji kutokana na changamoto za kibiashara.

"Wananchi wengi wa vijijini wamekuwa wakinunua mafuta kwa gharama kubwa na wakati mwingine kutoka kwa wauzaji wasio rasmi, jambo linaloongeza hatari za moto pamoja na kupanda kwa gharama za uzalishaji na usafirishaji,"amesema.

Ameongeza kuwa vituo vitakavyojengwa kupitia mpango huo vitafuata sheria, kanuni na viwango vya usalama vilivyowekwa na mamlaka husika ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na salama.

"Wanufaika 8 wa kwanza ndio watakuwa kioo cha mafanikio ya programu hiyo, huku akieleza kuwa serikali imeweka fedha za kutosha kwa ajili ya kuongeza idadi ya vituo vitakavyojengwa katika miaka ijayo," amesema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Nishati Jadidifu na Teknolojia za Nishati Mbadala kutoka REA, Mhandisi Advera Mwijage, alibainisha kuwa zaidi ya shilingi bilioni 12 zimetengwa na Serikali kufanikisha mpango huo kote nchini, ambapo kila mnufaika, ametengewa mkopo wa takribani shilingi milioni 133.